TANGAZO LA SERIKALI NA. 277 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 9(1) na (2))*

## NOTISI YA UANZISHWAJI (MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI BUNDA) YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Uanzishwaji (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Bunda) ya Mwaka 2023.

Inaanzishwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Sura ya 272

2.-(1) Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Bunda inaanzishwa kama Mamlaka ya Maji chini ya Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira na itakuwa na wajibu wa kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira katika mji wa Bunda.

(2) Haki, uwajibikaji, muda wa ajira, mali na madeni au masuala mengine yaliyotolewa au kufanywa na chombo au mamlaka nyingine ya maji na usafi wa mazingira katika mji wa Bunda, kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa Notisi hii yatakuwa chini ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Bunda.

Dodoma,
8 Machi, 2023

JUMAA H. AWESO
*Waziri wa Maji*